JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

TANGAZO

Tarehe: 09/03/2022

TANGAZO LA KAZI ZA UJENZI WA MRADI WA VYOO CHINI YA MRADI WA SRWSSP KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA SIKONGE KUANZIA MWEZI MARCH HADI APRIL MWAKA 2022

Ofisi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya ya Sikonge iliyopo Kijiji cha Mlogolo Kata ya Sikonge katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imepata fedha kwa ajili ya Ujenzi wa kuboresha Miundo mbinu ya vyoo chini ya Mradi wa *SRWSSP* kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.Kutokana na kupata fedha hizo ujenzi wa Matundu ya vyoo katika eneo la Mradi unatarajiwa kuanza Mwezi March na kukamilika Mwezi April Mwaka 2022.

Ujenzi wa Mradi huo ni kama ifuatavyo,

S/N	AINA YA MRADI	NAMBA YA MRADI
01	UJENZI WA MRADI WA VYOO MATUNDU 12	LGA/121/2021-2022/DH/01

Kwa kuwa njia ya ujenzi inayotumika ni ya kutumia wataalamu wa ndani na kununua vifaa **(Force Account);** Hivyo basi, Ofisi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya Sikonge inawatangazia wananchi wote wenye uwezo na sifa zilizotajwa hapo chini watume maombi yao kwa ajili ya Ujenzi huo:-

i. **Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka ishirini na moja (21) na asizidi miaka 55 na Mwenye Ujuzi na Uzoefu wa kazi za Ufundi Ujenzi anayeishi Mkoa wa Tabora ama Mikoa Jirani; (Mafundi wenye sifa wanaoishi Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Sikonge watapewa kipaumbele).**
ii. **Awe na uwezo wa kusoma na kutafasiri michoro, vipimo na uwiano wa vifaa vya ujenzi.**
iii. **Aeleze uzoefu alionao kwenye ujenzi hususani majengo ya umma .**

Scanned with CamScanner

iv. **Asiwe na historia ya kudhulumu, kutapeli au kutowalipa mafundi anaoshirikiana nao au kushindwa kukamilisha kazi alizowahi kupewa. Pia awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai au kufungwa jela.**

v. **Ajaze bei/gharama anazoomba kwa ajili ya kazi atakayoifanya (Schedule of labour)**

vi. **Awasilishe Mpango kazi wake,ukionyesha Mtiririko wa shughuli pamoja na muda atakaotumia ili kuzikamilisha**

vii. **Awe na vitendea kazi binafsi vya Mafundi kama vile Futi, Kamba, Pima maji nk.**

viii. **Awe na kikosi kazi cha Mafundi wasiopungua watano (5) na Wasaidizi wa fundi wasiopungua 5 hadi 10 kwa kazi anayoomba.**

ix. **Awe na uwezo wa kuwalipa mafundi na vibarua watakaomsaidia kazi kabla ya malipo yake kufanyika, malipo yatafanyika mara baada ya Mhandisi wa ujenzi (W) kuridhika na ubora wa kazi husika.**

x. **Awe na uzoefu wa kazi anayoiomba kwa muda usiopungua miaka 3 na aeleze Taasisi alizofanyia kazi, aonyeshe barua ya kupewa kazi (Letter of acceptance) au cheti cha kukamilisha kazi (Certificate of Completion). Nyaraka hizo ziambatanishwe kwenye barua ya maombi.**

Aina ya kazi zitakazofanyika:

A. Kufyatua tofali
B. Kujenga msingi wa jengo (sub structure)
C. Kunyanyua jengo (super structure)
D. Kuezeka (Roof structure and covering)
E. Kusimika fremu na kufunga milango na madirisha
F. Umaliziaji (Finishing)
G. Kupaka rangi na mapambo (Painting and decoration)
H. Ujenzi wa mashimo ya maji safi na taka (Water supply and sewage system)
I. Kuweka umeme (Electrical installation)
J. Kuweka mifumo ya maji safi na taka (Water supply and sewage system) kwenye majengo yote ya vyoo na kwenye mashimo ya maji taka

NB: (1) Kazi zilizotajwa hapo juu zitafanyika kwenye Maeneo Mawili tofauti ndani ya Hospitali ya Wilaya ya Sikonge kwa ujenzi wa Matundu sita (06) ya vyoo katika kila eneo litakaloamuliwa na Kamati ya ujenzi wa Mradi wa vyoo.

Scanned with CamScanner

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI KAMA IFUATAVYO;

i. Waombaji wanatakiwa kuja kuchukua BOQ Michoro ya kazi waliyoomba katika Ofisi Mganga Mganga Mfawidhi mara baada ya kulipia kiasi cha ***TZS. 10,000.00*** katika benki kupitia akaunti ya Hospitali ya Wilaya ya Sikonge ***51210013092 tawi la NMB***. **Risiti aliyolipia mwombaji iambatanishwe kwenye barua yake ya maombi.**

ii. Mwombaji anatakiwa kuainisha katika maombi yake Mradi anaoomba **(Mwombaji ataje jina na namba ya kazi aliyoomba)**

iii. Maombi yote yawekwe kwenye bahasha na kufungwa na juu ya bahasha iandikwe kazi iliyoombwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

iv. Vifaa vyote vitakavyotumika katika ujenzi husika vitanunuliwa na Ofisi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya ya Sikonge

v. Kamati ya ujenzi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhandisi ujenzi (W),itampitisha fundi mwenye vigezo kabla ya kufunga Mkataba.

vi. Barua ya Maombi iandikwe kwenda anwani ifuatayo;

Mwenyekiti Kamati ya Ujenzi wa Mradi wa vyoo,
Hospitali ya Wilaya,
S.L.P 70,
SIKONGE.

Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni tarehe 16/03/2022, Jumatano saa 7.00 mchana katika Ofisi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya Sikonge. Ufunguzi utafanyika muda huo. Waombaji au Wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi yao. Baada ya ufunguzi taratibu zingine za Manunuzi zitafuata.

Imetolewa na;

Selemani Pandawe
Mkurugenzi Mtendaji (W),
SIKONGE.

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE

Scanned with CamScanner